

KUISHI KATIKA NYUMBA YA WAKRISTO



BIBLE STUDIES FOR AFRICAN YOUTH

KUISHI KATIKA NYUMBA YA WAKRISTO

**Kimeandikwa na: Florence G. Chacha, Paul. G. Karani na
Robert Mutta**

BIBLE STUDIES FOR AFRICAN YOUTH

**Africa Coordinated Curriculum
for Bible Study**

Y1 - 3Ps

Used by permission of International Publication Services



**Published and Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
Box 30370, Nairobi**

©Copyright, 1990
Baptist Publications House
All Rights Reserved

kama hao wanapaswa kutoa ushuhuda mwema wa Kikristo mbele ya wazazi wao. Wanapaswa kumwomba Mungu awasadie kuwaonyesha wazazi wao njia ya kumwendea Kristo kupitia kwa tendo hili. Pengine itachukua muda kuwashawishi wazazi wao kwamba vijana hawa wanastahili kuwa mume na mke. Litakuwa jambo muhimu kujaribu kupata baraka za wazazi wa pande zote mbili.

Ni muhimu kufanya mambo yote jinsi tunavyofundishwa katika 2 Timotheo 2:15, "Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli."

KAZI YA KUFANYA

1. Fikiria jinsi utakavyo mpata mchumba wako wa ndoa. Je! utataka ushauri wa nani?
2. Ifikirie jamaa yako. Je! ni ushuhuda gani utakaoutoa kuwasaidia kumkaribia Mungu?
3. Je! kwa nini ni muhimu kwako kuwaheshimu wazazi wako katika shughuli za kumtafuta mchumba?
4. Omba kwamba wakati wa ndoa yako utakapofika utakuwa tayari kumtegemea Bwana kwa kila jambo.

YALIYOMO

SURA

UKURASA

1. Mpango wa Mungu kwa Nyumba Kamilifu. 5
2. Mwanadamu Aliamua Kubadili Mpango wa Mungu. 8
3. Yesu Anamkumbusha Mwanadamu Mpango wa Mungu.. 13
4. Maisha ya Mkristo Nyumbani. 16
5. Amri za Mungu kwa Mume. 21
6. Amri za Mungu kwa Mke. 25
7. Ushirikiano wa Mume na Mke. 29
8. Malengo ya Wazazi kwa Watoto Wao. 33
9. Je! Ni Nani Anayestahili Kuwalea na Kuwarudi Watoto. 37
10. Ibada ya Jamaa. 42
11. Amri za Mungu kwa Mtoto. 46
12. Je! Nitamwoa Nani? 50
13. Je! Ni nani Anayepaswa Kunichagulia Mchumba? 55

KUHUSU WAANDISHI

Mrs. Florence G. Chacha ni mke wa mchungaji huko Nairobi, Kenya ambaye ana ujuzi wa kufanya kazi na vijana. Amepata elimu ya theologia na kwa sasa yuko katika chuo cha ualimu.

Paul G. Karani ni mwalimu wa masomo ya watu wazima, ambaye pia anawafundisha vijana huko Malindi, Kenya. Yeye ni mshiriki wa Ziyabomu Baptist Church.

Robert Mutta ni mfanya kazi wa Baptist Publications House, Nairobi, katika idara ya uhariri. Huwafundisha vijana wa Kahawa West Baptist Church. Anayo shahada ya diploma katika theologia kutoka chuo cha International Baptist Theological Seminary of Eastern Africa. Robert Mutta ni Mtanзания.

mwanadamu na watu wengine. Hii inaonyesha kwamba amri hii ni muhimu sana. Malizia kusoma kifungu hiki kutoka katika Biblia. Kinatwambia kwamba siku zetu zitakuwa nyingi tunapowahishimu wazazi wetu. Hii ndiyo ahadi ya maisha maretu tukitii amri hii.

Wazazi wanapaswa kuheshimiwa hata katika ndoa. Tunasoma katika Mwanzo 24:28 kwamba Rebeka alienda mbio na kuwaambia wazazi wake wakati mtumishi wa Ibrahimu alipotunwa kumtafutia Isaka mke naye akakutana na Rebeka na kumwelezea hivyo. Rebeka hakuitiambia ndoa yake na Isaka kuwa ya siri au jambo la binafsi. Alilitiambia jambo hili kuwa wazi na kuwahusisha wazazi wake. Tunaona katika kifungu cha 50 na 51 kwamba Laban na Bethueli walimrhusu mtumishi yule kumpeleka Rebeka kwa bwana wake. Hawapinga ndoa yao. Wazazi hawapaswi kupinga ndoa za watoto wao bila sababu maalum. Soma Waefero 6:4. Wazazi wanapaswa kuheshimiwa, nao wanapaswa kushirikiana na watoto wao ili kila mmoja awe na furaha.

MAFUNZO YA SURA HII KWANGU

Vijana wanaotaka kua wanapaswa kushirikiana na wazazi wao ili kila mmoja afurahie ndoa yao. Wanapaswa kuomba pamoja na kumwomba Mungu awaongoze katika uamuzi huu muhimu. Ndipo ndoa hiyo itakuwa yenye msingi wa Mungu. Uamuzi wote utafanywa kwa njia ya kumheshimu Mungu na kuleta furaha kama wazazi wote wanatafuta kufanya mapenzi ya Mungu na kutaka kumtumika.

Jei itakuwaje kama mmoja wao si Mkristo? Soma tena sura ya kumi na mbili ya kitabu hiki ikiwa umesahanu mafundisho yake. Soma pia 2 Wakorintho 6:14-16.

Jei itakuwaje kama yule mnyulana au msichana anatoka katika jamaa ya wasio Wakristo? Hii ni kwele mara nyingi. Vijana

Hatimaye Yakobo alienda nyumbani kwao pamoja naye kuchukua nguo zake. Akamwambia babake kwamba amemwoa Susanna.

Susanna na Yakobo walikuwa wameanza maisha ya ndoa bila wazazi wao kujua. Hawakuwatii wazazi wao walipofanya hivi wala hawakupokea baraka zao kwa ndoa yao. Hawakumwomba Mungu awe sehemu ya ndoa yao.

MAELEZO

Tumeona katika hadithi hii kwamba Yakobo na Susanna hawakumhusisha Mungu wala wazazi wao katika ndoa yao. Mungu anapaswa kuwa wa kwanza maishani mwetu. Ametuahidi maisha ya baadaye na matumaini. Ametupa haki ya kumwomba tukijua kwamba anatusikiliza.

Je! Mungu anataka tufanye nini? Anataka tumtafute kwa bidii. Ni lazima tumtafute kwa moyo wetu wote. Ni lazima tujitahidi kumjua na kufanya mapenzi yake. Ndipo tutaona mapenzi yake.

Tunapomchagua mchumba huwa tunafanya uamuzi ambao utahusu maisha yetu yote. Tutateseka daima kama hatutamhusisha Mungu katika jambo hili muhimu. Ni lazima Mungu awe wa kwanza. Ni lazima tumtii kuliko mtu mwingine ye yote.

"Nyumba na mali ni urithi apatao mtu kwa babaye, bali mke mwenye busara, mtu hupewa na Bwana" (Mithali 19:14).

Susanna aliwadharau wazazi wake. Hivyo ni kuvunja amri ya Mungu. Kutoka 20:12 inasema, "Waheshimu baba yako na mama yako...."

Unapaswa kumheshimu mtu ye yote ambaye ni mkubwa kwako. Amri hii inasema uwaheshimu wazazi wote wawili. Hii ndiyo amri ya kwanza ya Mungu inayohusu ushirika wa

SURA YA KWANZA MPANGO WA MUNGU KWA NYUMBA KAMILIFU

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba Mungu alipanga kuana kwa mume mmoja na mke mmoja.

SOMO KUTOKA: Mwanzo 2:18-24

VIFUNGU VYA LEO: Mwanzo 2:18-24

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja" (Mwanzo 2:24).

KUSOMA SOMO

UTANGULIZI

Yakobo alitambua kwama hana koti la kuvaa wakati wa majira ya baridi. Baba yake alikuwa amemnunulia aina nyingine za nguo. Alimnunulia pia vifaa vya shule ambavyo vilihitajika na baisikeli ya kuendea shuleni. Yakobo hakufurahi hata ingawa baba yake alimnunulia vitu vya kumsaidia.

Baba yake alienda dukani na akamnunulia koti. Yakobo alifurahi sana alipoona koti hilo. Alifikiri kwamba hataisia baridi atakapolivaa.

Adamu hakuwa mwenye furaha hata ingawa Mungu alimpatia vitu vingi katika bustani ya Edeni. Adamu hakufurahi kwa sababu hakuwa na msaidizi. Hebu sasa tujifunze habari yake.

MAELEZO

Mungu alimwumba mwanadamu kwa mavumbi ya ardhi. Aliwaumba pia viumbe wenye uhai, ng'ombe na kila kitu kitambaacho juu ya nchi. Mungu alimletea mwanadamu vitu

hivi ili avile majina. Yule mwanadamu, Adamu, alivipa majina viumbe hivi vya Mungu, lakini hapakuwa na kile ambacho wangeshirikiana. Wanyama wangemaidia mwanadamu kwa kazi yake, lakini hawatashirikiana naye jinsi anavyotaka.

"Bwana Mungu akasema, Si vyema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye" (Mwanzo 2:18). Mungu hakuwa amemaliza kazi yake hata ingawa alikuwa amemfanyia Adamu mengi. Adamu alihitaji mtu ambaye angotosheleza hamu moyo wake. Adamu na msaidizi huyo wangeonyeshana upendo, wangepaminiana na kusikilizana katika maisha yao ya jamaa.

Tunaambiwa katika kifungu cha 21 kwamba Adamu alipata usingizi mzito. Mungu alitumia usingizi huu mzito kufanya mwujiza ambao ulileta kiumba na Adamu. Mungu alichukua ubavu mmoja kutoka kwa Adamu kisha akafunika nyama mahali pake. Alifanya kiumba mwingine kutoka kwa ubavu huo, ambaye Adamu alimwita mwanamke.

Mungu alimpa Adamu kiumba huyo mpya baada ya kumaliza kumwumba. Mungu alianzisha mpango kamili kati ya mume na mke. Watu hawa walipaswa kupendana, kutunzana, kuaminiana na kusaidiana wakati wote maishani.

Adamu alifurahi na akatosheka baada ya Mungu kumwumba mwanamke. "Adamu akasema, 'Sasa huyu ni mfuja katika mifuja yangu, na nyama katika nyama yangu...' (Mwanzo 2:23). Adamu alijisikia kwamba mwanamke huyu alikuwa sehemu ya mwili wake na alipaswa kumpenda jinsi anavyojipenda.

Tunaona katika kifungu cha 24 kwamba watu wawili wataishi pamoja kama mwili mmoja. Wataanzisha nyumba nao watakuwa vyombo vya Mungu vya kuikuza jamaa hiyo ipate

SURA YA KUMI NA TATU JE! NI NANI ANAYEPASWA KUNICHAGULIA MCHUMBA?

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kumtegemea Mungu kunichagulia mchumba, lakini nitawaheshimu wazazi wangu katika mambo yote pamoja na jambo hili muhimu.

SOMO KUTOKA: Kutoka 20:12; Yereemia 29:11-13

VIFUNGU VYA LEO: Kutoka 20:12; Yereemia 29:11-13

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Lakini mwenendo wenu na uwe kama inavyoipasa Ijili ya Kristo, ili, nikija na kuwaona ninyi, au nisipokuwapo, niyasikie mambo yenu, kama mmasimama imara katika roho moja, kwa moyo mmoja mkishindania imani ya Ijili" (Wafilipi 1:27).

KUSOMA SOMO

UTANGULIZI

Susanna aliishi nyumbani na kwenda shule ya sekondari ambayo haikuwa mbali na kwao. Yakobo alitoka mjini ambako aliishi katika nyumba ndogo. Alifanya kazi wakati alipohitaji pesa, lakini hakudumu kwa kazi aliyopata.

Wakati mwingine Yakobo alimchukua Susanna na kwenda kutembea katika gari lake huku wengine wakiwa darasani. Walikwenda nyumbani kwake na kutaka huko kwa saa nyingi. Hatimaye alipendezwa sana na Yakobo na mwenendo wake kuliko kazi ya shule. Aliendelea kushindwa na masomo jinsi alivyokosa kuhudhuria shule.

Yakobo na Susanna waliamua siku moja kuishi pamoja kama mke na mume. Hawakuwaambia wazazi wao, na iliwachukua wazazi wa Susanna siku mne kujua mahali alipokuwa.

"Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako" (Kutoka 20:12).

Mume na mke wanapaswa kumtanguiza Kristo maishani mwao. Kulingana na Mwanzo 24:50-51, 58, Rebeka na jamaa yake walijua kwamba ulikuwa mpango wa Mungu kwamba aolewe na Isaka. Kwa hivyo hawakumkataza mtumishi wa Ibrahimu. Mkristo anapaswa kuelewa mapenzi ya Mungu na awe tayari kumtanguiza, anapotaka mchumba kabla na baada ya kuoana. Yesu amesema kwamba, "Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa" (Mathayo 6:33).

Ni katika Yesu tu ambako ndoa kamili inaweza kupatikana.

KAZI YA KUFANYA

1. Je! unapaswa kuangalia mambo yapi unapomfikiria yule utakaye mwoa? Andika orodha ya mambo haya.
2. Je! ni muhimu kumwoa mwenyeji wa nchi yako? Na kabila lako je?
3. Je! ni muhimu kumwabudu yule mnayeabudu pamoja? Kwa nini?
4. Mwombe Mungu akuongoze kumpata mchumba anayekufaa kwa ajili ya utukufu wake.

kumpendeza. Kuambatana huku kungekuwa kwa milele. Hawangetenganishwa maisha yao yote.

MAFUNZO YA SURA HII KWANGU

Mungu alimwumba Adamu, baada ya kuumba mbingu na nchi na vyote vilivyomo. Alisema kwamba mwanadamu angetumia vitu hivyo vyote, lakini haviikutosheleza Adamu. Kisha Mungu alimfanyia msaidizi na akamletea. Mungu ndiye aliyepanga nyumba kamilifu. Mume mmoja na mke mmoja wangeishi pamoja katika maisha yao yote.

Tunapomhitaji mtu wa kutufariji na kutuonyesha upendo, ni lazima tuombe mapenzi ya Mungu yafanyike. Ni lazima Wakristo wamngojee Mungu awape mwenzi. Anajua tunawahitaji lakini hatuwezi kuwapata sisi wenyewe. Biblia inatufundisha katika Mithali 19:14, "Nyumba na mali ni urithi apatao mtu kwa babaye; Bali mke mwenye busara, mtu hupewa na Bwana."

Mungu alianzisha nyumba ya watu wawili. Alimwumba mwanamume mmoja na mwanamke mmoja aliyefanywa kuwa mke wa Adamu. Wakristo hawapaswi kumwoa mke zaidi ya mmoja. Lazima wawe jamaa moja mara tu wanapooana. Biblia inatwambia, "...mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja" (Mwanzo 2:24). Wakati mwanamume na mwanamke wanapowaacha wazazi wao huanzisha nyumba. Wanaweza kuitunza nyumba yao na kuamua watakachofanya kumtumikia Bwana. Wanapaswa kuwasaidia wazazi wao wakiwa na shida, lakini wao hufanyika jamaa mpya.

Mungu aliwaweka Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni. Alitaka pawe makao yao. Hakuwaamulia kila jambo. Walikuwa na wajibu wa kufanya kazi ya kutunza bustani hiyo.

Kwa hivyo, ni mpango wa Mungu kwamba kila jamaa jitunze yenyewe.

Adamu alifurahi sana alipoletewa msaidizi. Soma Mwanzo 2:23. Watu wawili hufurahi wanapunganishwa kama mume na mke. Ni lazima wawe vyombo vya Mungu na wantumikie kwa utukufu wake katika furaha yao. Wanapaswa kuishi pamoja milele. Yesu alisema, "...Basi aliwauunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe" (Mathayo 19:6b). Kuunganishwa huku kunapaswa kutenganishwa na kifo tu.

KAZI YA KUFANYA

1. Mshukuru Mungu kwa kumwumba mwanamume na mwanamke.
2. Mwombe Mungu akupe subira ili mapenzi yake yatimizwe maishani mwako.
3. Omba kwamba Mungu atakupatia mke au mume aliyekuchagua jinsi alivyomfanyia Adamu.

SURA YA PILI

MWANADAMU ALIAMUA KUBADILI

MPANGO WA MUNGU

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba mateso mengi huja wakati wanadamu wanapokosa kumtii Mungu.

SOMO KUTOKA: 2 Samweli 12:2-27

VIFUNGU VYA LEO: 2 Samweli 12:2-5, 14, 26-27

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Nimekutenda dhambi Wewe peke yako, Na kufanya maovu mbele za macho yako..." (Zaburi 51:4a).

lakini wao walikuwa wa ulimwengu. Katika Utangulizi wetu wa leo tunaona jinsi Sara alivyofanya kosa la kiolewa na Yohana kwa sababu ya umbo lake na mambo mema aliyomfanyia. Hii iilisababisha kuvunjika kwa mapenzi yao. Watu wawili wenye imani na tabia tofauti hawawezaji kuishi pamoja. Biblia inasema, "Usilime kwa ng'ombe na punda wakikokota jembe pamoja" (Kumbukumbu la Torai 22:10).

Baadhi ya watu huoana na wasio Wakristo wakitumainia kwamba siku moja watabadili imani yao. Hii ni kinyume cha mafundisho ya Biblia. Wakristo wameambiwa katika 2 Wakorintho 6:17 kujitenga na wasio Wakristo, naye Mungu atawakaribisha kwake.

MAFUNZO YA SURA HII KWANGU

Wale wanaotarajia kuoa ni lazima waishi maisha safi mbele za Mungu. Mungu alimleta msichana mrembo aliyekuwa bikira wakati mtumishi wa Ibrahimu alipongojea kisimani. Rebeka alikuwa amejikwa safi kwa sababu alitaka kumpendeza Mungu kuliko wanadamu.

Waebrania 13:4 inafundisha kwamba, "Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi, kwa maana washherati na wazinzaji Mungu atawahukumuia adhabu." Ni lazima Mkristo ambeshimu Mungu, ili awe msafi mbele zake.

Msichana yule alikuwa tayari kuvapa ngamia maji wakati mtumishi wa Ibrahimu alipomwomba maji ya kuuuya. Hii inaonyesha kwamba Rebeka alikuwa mkarimu na jirani mwema. Alikuwa pia mwenye hekima, mjasiri na mwenye nia njema. Wanaonua kuoana wanapaswa kuwa na tabia sawa.

Jambo lingine la kuangalia ni jinsi mwenzako anavyowatendea wazazi wake. Rebeka alipopata habari aliwaendea jamaa na kuwapasha habari. Rebeka aliwatii wazazi wake hata katika ndoa. Hivi ndivyo inavyopaswa kuwa kwa kila mmoja.

ngamia kumi na kwenda mpaka Mesopotamia. Alipofika kisimani, alimwomba Bwana atimize ahadi aliyomfanyia bwana wake. Tunaona katika vifungu vya 16-28 kwamba Mungu alimleta msichana mrembo aliyekuwa bikira. Msichana huyu alijaza maji mtungi wake. Mtumishi huyu alitaka maji ya kunywa, naye yule msichana akampa maji ya kumtoshia pamoja na ngamia zake. Mtumishi alipoona mambo haya, alimpa msichana huyo, Rebeka, pete ya dhahabu na vikuku viwili (bangili). Rebeka alijua kwamba Mungu anafanya mwujiza maishani mwake, na akaenda kuwaambia watu wa nyumba yake habari hii.

Tunaona katika vifungu vya 50 hadi 61 kwamba jamaa ya Rebeka walitaka kumfanya Mungu kuwa wa kwanza wakati mtumishi wa Ibrahimu alipoenda nyumbani kwao. Walijua yalikuwa mapenzi ya Mungu, wala hawakusita. Rebeka alimfuata mtumishi wa Ibrahimu hadi kwa mumewe, Isaka. Isaka alimpenda sana Rebeka.

Ibrahimu alimwamini Mungu alipomtakia mwanawe mke. Alimwambia mtumishi wake kwamba Mungu atamtafutia mwanawe mke. Ni lazima mtu ye yote anayetaka kuoa amini kwamba Mungu atampatia mchumba. Mungu aliyempa Adamu humpa kila mtu. Biblia inafundisha kwamba tunaweza kurithi vitu vingi kutoka kwa baba zetu, lakini tunaweza tu kupata mwenzi wa maisha kutoka kwa Mungu. Soma Mithali 19:14.

Ibrahimu alimtakia mwanawe aoe mke wa nyumbani kwao, mtu mwenye nia moja naye. Watu wanaoana wanapaswa kuwa wenye imani moja na malengo sawa. Paulo anasema katika 2 Wakorintho 6:14-16 kwamba Wakristo hawapaswi kufungwa nira pamoja na wasioamini jinsi nuru na giza isivyoweza kushirikishwa pamoja. Tunaona katika Mwanzo 24 kwamba Isaka angewapata wasichana wengi pale Kanaani na kuwaoa,

KUSOMA SOMO UTANGULIZI

Mtu mmoja alikuwa na mwana aitwaye Yusufu, na aliyependa sana. Mtu huyu alijua mahitaji ya mwanawe na akampatia cho chote alichohitaji. Hata hivyo, mwanawe alikuwa mchonyo na mwenye wivu, na alitaka apewe kila kitu alichoona. Siku moja aliona mfuko wa mtu mwingine na akauchukua bila kujali kwamba ana mfuko mingine kama huo nyumbani. Mfuko huo ulikuwa wa mtu aliyefanya biashara ya kuuza nyoka. Yusufu hakujua la kufanya alipoufungua mfuko huo, kwani nyoka alitoka na kumwuma.

Baba ya Yusufu alikasirika sana kwa kuwa Yusufu alikuwa na mfuko mingi aliyohitaji. Alipata shida kwa sababu ya uchoyo na wivu wake kwa kuwa hakufuata mipango ya baba yake.

Kuna watu katika Agano la Kale ambao hawakufuata mpango wa Mungu na wakapata taabu. Hebu tujifunze baadhi yao.

MAELEZO

Daudi alikuwa mfalme wa Israeli kwa muda wa miaka arobaini. Kulikuwepo na vita vingi wakati wa utawala wake, na alihakikisha kwamba maadui wote wa Israeli wameangamizwa. Alikuwa mfalme mwenye uwezo mkuu. Lakini katika kilele cha utawala wake, alizini na Bathsheba, mke wa mmoja wapo wa maafisa wake.

Daudi alikuwa amemtuma Yoabu, watumishi wake na Waisraeli wote kuangamiza Amoni na kuteka Raba, wakati yeye alibaki Yerusalemu. Siku moja jioni alipokuwa akitembea juu ya dari ya nyumba yake alimwona mwanamke akioga. Akamwona kuwa mzuri sana. Daudi alitaka kujua ni nani huyo. Akaambiwa kwamba ni Bathsheba mkewe Uriah, Mhiti. Akawatuma watu wakamlete kwake. Daudi akalala naye.

Akafanya dhambi kwa tendo hii. Inaonekana kwamba Bathsheba hakukataa kwani alitikia mwito wa mfalme, wala hakusia.

Mwanamke huyu alirudi nyumbani baada ya dhambi hii. Tunaona katika kifungu cha 5 kwamba mwanamke huyu alichukua mimba na akampelekea Daudi ujumbe kwamba ni mja mzito. Daudi alijua kwamba ataibika wakati Uria atakapojua kilichofanyika. Daudi alimpenda sana mwanamke huyo hata ingawa alikuwa na wake wengine wengi.

Daudi aliamuru kwamba Uria aje Yerusalemu. Alitaka akae na mkeke ili ionekane kwamba mtoto huyo ni wake. Lakini Uria alilala nyumbani kwa watumishi wake badala ya kwenda nyumbani kwake. Alisema kwamba rafiki zake wanapigana naye hawezi kwenda nyumbani kwake wakati huu akafurahi. Daudi alimfanya alewe ili akalale nyumbani, lakini hakufaulu.

Daudi alimpatia Uria barua ampelekee Yoabu. Barua hii ilimsauri Yoabu amweke Uria mbele penye vita vikali. Uria na watumishi wengine wa Daudi walikufa vita vilipoanza. Daudi alitaka Uria afie vitani ili asishutumiwe kwa ajili ya kifo chake.

Tunasoma katika vifungu vya 26-27 kwamba ujumbe ulimfikia mkeke Uria na akamwombolezea mumewe. Daudi alimchukua Bathsheba na kuwa mkeke baada ya kumaliza maombolezo. Naye akamzaa mwana wa kiume. Tunasoma katika 2 Samweli 12:15-18 kwamba Mungu hakumwacha mtoto huyo aishi. Mtoto huyo alikufa kwa sababu ya dhambi ambayo Daudi alimfanya Bwana. Dhambi hii ilimfanya Daudi atambue kwamba yuko mbali na Mungu. Matokeo ya dhambi yake yalionekana hata ingawa aliomba msamaha, akafunga na kutia.

Mungu amekataza kutwa mke wa mtu mwingine. Bathsheba alikuwa mke wa mtu mwingine, na Daudi hakupaswa kamwe

kuwa Bwana na Mwokozi wake. Alikuwa amemaliza masomo yake akiwa na miaka ishirini na mbili na alikuwa amejirirwa mimi kama mwandishi. Alikutana hapo na Yohana, mfanya kazi mwenzake.

Yohana aliahidi kumwoa Sara. Sara alipendezwa sana na kijana huyu, na akijisikia mpweke alipokuwa hayuko karibu. Alifurahia tu kuwa pamoja naye. Yohana hakuwa Mkristo, lakini alikuwa tajiri sana. Alionekana mwenye umbo zuri na kufanya mashauri mema. Alikuwa akimpeleka Sara mahali pa starehe kila wakati. "Pengine atakuwa Mkristo baada ya kunioa," Sara akawaza. "Kisha tutamtumikia Bwana pamoja."

Walioana baada ya miaka miwili. Lakini wakaanza kuwa na shida. Watu wawili ambao walikuwa wenye tabia na imani tofauti hawangeishi pamoja kwa furaha.

MAELEZO

Ndoa ni mpango wa Mungu, na wote wanaotaka kuoa ni lazima wajue yale ambayo Mungu anataka wafanye. Mtume Paulo aliandika kuhusu ukweli muhimu ambao haupaswi kupuuzwa tunapochagua mwenzi wa maisha. Anasema kwamba hatupaswi kuunganishwa na wasio waamini. Tunapaswa kuoa watu wenye imani sawa na yetu.

Tunaweza kupata mambo mengi katika Mwanzo 24 ambayo tunapaswa kufikiria kabla ya kuoa. Ibrahimu alimtaka mwanawe Isaka akatafute mke kutoka nyumbani kwao, mahali alipozaliwa. Mtumishi alitumwa naye akamletea Isaka mke kutoka huko. Ibrahimu alimtaka Isaka amwoc mke mwenye lengo sawa naye na mwenye mawazo kama yake badala ya kumwoa mgeni.

Tunaona katika kifungu cha 6 kwamba Ibrahimu aliamini kwamba Bwana atampatia mwanawe mke, hata kabla ya mtumishi wake kuanza safari. Mtumishi, huyo alichukua

KAZI YA KUFANYA

1. Soma Kifungu cha Kukumbuka kila siku kabla ya kulala, na ujifunze kukikariri.
2. Je! unaweza kukumbuka wakati ulipowatii wazazi wako, wakati ulipotaka kufanya jambo fulani tofauti? Je! ni nini kilichofanyika?
3. Mwombe Mungu akusaidie kuwatii wazazi wako na akusamehe pale ulipokosea.

SURA YA KUMI NA MBILI JE! NITAMWOA NANI?

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba Mungu ana mpango kamili kwa maisha yangu, na ataniongoza katika kuchagua mwenzi.

SOMO KUTOKA: 2 Wakorintho 6:14-15; Mwanzo 24; Waebrania 13:4

VIFUNGU VYA LEO: 2 Wakorintho 6:14-15; Mwanzo 24; Waebrania 13:4

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza?" (2 Wakorintho 6:14)

KUSOMA SOMO UTANGULIZI

Sara alikuwa msichana mrembo alipoolewa akiwa na miaka ishirini na minne. Wazazi wake walikuwa Wakristo, naye alikuwa amekiri mbele ya kanisa kwamba atamfuata Kristo

kujishughulisha naye. Lakini Daudi aliamua kubadili mpango wa Mungu. Tuone sasa ni yapi ambayo Mungu anatwambia leo hii.

MAFUNZO YA SURA HII KWANGU

Mara kwa mara mwanadamu ameweza kudharau amri za Mungu na kubadili yale ambayo Mungu amempangia. Hii inasababishwa na tamaa mbovu za moyo na mwili wake.

Daudi alikuwa na wake wengi jinsi ilivyoandikwa katika 2 Samweli 12:8, lakini hakutosheka nao. Alimchukua tena Bathsheba, mke wa Uria na kumfanya mkewe. Daudi alifanya kinyume na mpango wa Mungu, akajiletea taabu.

Ibrahimu na Sara pia walipata shida walipoamua kupata mtoto kupitia kwa Hajiri. Soma Mwanzo 16 na Mwanzo 21:9-21. Mungu alikuwa amemwahidi Ibrahimu kuwa Sara atamzalia mwana. Sara hakuamini kwa kuwa walikuwa wazee sana. Sara akamwambia Ibrahimu kwamba amtwae Hajiri kama mkewe. "Basi akamwingilia Hajiri, naye akapata mimba. Naye alipoona ya kwamba amepata mimba, bibi yake alikuwa duni machoni pake" (Mwanzo 16:4). Uhusiano ulidhoofika kati ya Sara na Hajiri baada ya kufanya tendo hili na kutomtii Mungu. Lakini Sara alipozaa mwana baadaye akamwambia Ibrahimu, "...Mfukuze mjakazi huyu na mwanawe, maana mwana wa mjakazi hatarithi pamoja na mwanangu, Isaka" (Mwanzo 21:10).

Watu wengine wa Agano la Kale walikataa amri za Mungu kwa kuoa mke zaidi ya mmoja. Hatupaswi kufuata mfano wao. Mungu alimwumba mwanamume mmoja na mwanamke mmoja kuwa jamaa ya kwanza. Alitaka watu wake waishi hivyo daima. Shida huja tunapokataa kumtii Mungu. Wakristo pia watapata shida wakibadilisha mpango wa Mungu na kuoa

wake wengi. Mungu habadiliki kamwe. "Kwa kuwa mimi, Bwana, sina kigeugeu..." (Malaki 3:6a).

Mungu alimwumba mwanamume mmoja na mwanamke mmoja kuishi pamoja kama mume na mke katika bustani ya Edeni. Mungu alitaka waishi pamoja kwa upendo na amani. Yesu alisema, "...na hao wawili watakuwa mwili mmoja" (Mathayo 19:5b). Hakusema hao watatu wala wanne, bali hao wawili.

Wakristo hawapaswi kuishi kulingana na matendo ya waliowatangulia. Tunapojua mpango wa Mungu, tunapaswa kuishi kama Wakristo wa kweli na kufuata mpango wake maishani mwetu. Biblia inatufundisha kwamba, "Lakini aliyetazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake" (Yakobo 1:25).

Mapenzi ya Mungu hayabadiliki. Yeye hudhirisha mapenzi yake katika Neno lake.

KAZI YA KUFANYA

1. Mwombe Mungu akusaidie kuwa mwenzi anayefaa wakati wako utakapofika.
2. Jitoe kwa Mungu na kumwambia kwamba utakuwa tu na mume au mke mmoja.

MAFUNZO YA SURA HII KWANGU

Hebu fikiria baadhi ya mambo ambayo wazazi wako walikufanyia ulipokuwa mdogo. Walikupa chakula, nguo, karo ya shule, dawa na vitu vingine. Walikutunza ili usipate na madhara na wakafundisha mambo mengi kuhusu maisha.

Fikiria tena jinsi unavyotenda ukiwa na wazazi wako. Je! huwa unawathamini vya kutosha? Je! ni njia ipi bora ambayo utatumia kuwaonyesha shukrani zako kwa yote walivyokufanyia? Ni kwa kuwatii na kuwakeshimu.

Kuna njia kadhaa ambazo unaweza kutumia kuwaonyesha shukrani zako. Unaweza kwenda nyumbani na kuwasaidia na kazi za nyumbani wakati mapofunga shule. Unaweza kutunza na kutumia vitu ambavyo wamekupatia. Hata kazi yako ya shuleni inaweza kuonyesha shukrani zako kwa kujitolea kwa wazazi wako ili upate kwenda shuleni. Je! unajitahidi katika masomo yako? Huu ndio wakati wa kutayarisha maisha yako ya baadaye. Unaweza kuonyesha shukrani zako kwa wazazi wako ikiwa utatumia vizuri muda wako.

Ni lazima uwatii kwa kwenda po pote wanapokutuma na kufanya kile unachoambiwa. Unapaswa kutii maonyo ya wazazi wako. Tumeona katika Utangulizi kwamba wana wa Eli hawangekufu kama wangepii maonyo ya baba yao juu ya kutenda maovu katika nyumba ya Bwana. Wazazi wako wanapokuonya juu ya jambo fulani, huwa wamejua hatari na madhara yake. Ni muhimu kwa watoto kuwasiliza wazazi na kuwatii. Wanaweza kuwa wamezeeka, au pengine hawajasoma, lakini wanayo hekima kuu. Zaidi ya hayo, Mungu amewaamuru watoto wawatii wazazi wao. Si jambo la watoto kuamua kufanya. Ni amri ya Mungu. Mwanafunzi huanguka mihani wake anapokosa kufuata maagizo aliyopewa. Je! itakuwaje kwa wale ambao wamekosa kutii maagizo ya Mungu ya kuwatii wazazi wao?

wanawe wawili watakufa siku moja. Soma 1 Samweli 4 kuona jinsi wana hao wawili walivyokufa katika vita vyao na Wafilisti. Kutotii ni dhambi na mshahara wa dhambi ni mauti.

MAELEZO

Mungu hakubali kamwe kutotii. Ni muhimu kutii. Waisraeli waliadhibiwa na Mungu kila mara walipokosa kumtii katika safari yao ya kwenda Kanaani. Yona alilala tumboni mwa Samaki siku tatu usiku na mchana alipokataa kumtii Mungu. Yona alisema kwamba hapakuwa mahali pazuri pa kukaa.

Watoto wameamriwa katika Waefeso 6:1-3 kuwatii wazazi wao. Hii ndiyo haki yao. Hili ni tendo jema. Watoto wameambiwa wawatii baba zao na mama zao. Hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi. Watafanikiwa maishani wakiwatii nao wataishi siku nyingi duniani. Watoto wanapaswa kuwatii wazazi wao katika mambo yote, kwani jambo hili humpendeza Mungu. (Soma Wakolosai 3:20.)

Kuwa mtiifu kwa wazazi humwelekeza mtu kwa Mungu ambaye huleta amani, furaha na mafanikio maishani. Hili ndilo lengo la kila mtu tangu utotoni. Yesu alirudi Nazareti na wazazi wake baada ya kuwa hekaluni, na akawa akiwatii. (Luka 2:51)

Watoto wanapaswa kuwatii na kuwaheshimu wazazi wao kwani ndiyo haki yao. Ni amri ya watoto wote. Wazazi wapo kuwaongoza, kwa hivyo wanapaswa kufuata mashauri yao.

Kutotii huleta huzuni na majuto. Ni lazima uwasikilize na uwatii wazazi wako kama unataka kuwa mtu mwema na mwaminifu katika jamii yako. Mithali 13:1 inatwambia kwamba mwana mwenye hekima husikiliza mausia ya watu wengine.

SURA YA TATU

YESU ANAMKUMBUSHA MWANADAMU MPANGO WA MUNGU

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba Yesu alimkumbusha mwanadamu juu ya mpango wa Mungu wa ndoa.

SOMO KUTOKA: Mathayo 19:4-6; Marko 10:2-12; Waefeso 5:31

VIFUNGU VYA LEO: Mathayo 19:4-6; Marko 10:2-12; Waefeso 5:31

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja" (Waefeso 5:31).

KUSOMA SOMO

UTANGULIZI

Yoshua aliondoka nyumbani kwenda kusaidia kanisa la wilaya nyingine. Wakati akiwa njiani kurudi nyumbani baada ya wiki moja, alifikiria jinsi anavyokwenda kuungana na jamaa yake. Lakini furaha yake iliisha alipofika nyumbani na kugundua kwamba mkewe hakuwa mwaminifu yeye alipokuwa mbali naye.

Yoshua alikasirika sana, akasema kwamba hatamsamehe mkewe kwa jambo hilo. Aliamua mara moja kwamba suluhisho lake ni kumpa talaka.

Watu wengi waliooana wametumia talaka kama suluhisho la kutopatana kwao. Hebu tujifunze Mungu anataka tufanye nini wakati kama huu.

MAELEZO

Yesu alikuwa anafundisha Mafarisayo walipoingia Yuda, ng'ambo ya Yordani ili kumjaribu. Walikuwa wamejiifunza shuleni kwao kwamba mume angemfukuza mkewe kwa sababu nyingi. Hawakujua kwamba Mungu alipanga mume na mke kuishi pamoja mtlele.

Mwanadamu alipadili mpango wa Mungu kwa kuwaoa wake wengi. Mfano ni Ibrahimu, Daudi, Sulemani na wengine wengi katika Agano la Kale walionyesha kwamba shida hiyo ilikuwepo. Wanaume na wanawake wengi walishindwa kuishi kwa uaminifu katika ndoa, kukawepo uzinzi na usherati mwingi. Talaka ndiyo iliyofikiwa kwa suluhisho la shida nyingi zilizoipata jamaa. Musa aliwaamuru kutoa talaka kwa sababu ya ugonvu wa mioyo yao. Soma Kumbukumbu la Torati 24:1-4. Musa alifanya hivyo kwa manufaa ya mwanawake. Alitaka kumwoko asitendewa maovu kwa kuwa talaka haikuwa imekubaliwa. Talaka iliyoruhusiwa ilikuwa ya lazima.

Mafarisayo walipofika kumtega Yesu, alipuza mabishano ya shule zao. Maelezo yake yalipita sheria za Musa na akazungumzia kusudi la sheria ya Mungu. Mungu alendelea kudai uti wa Israeli, na walipaswa kumtumikia kwa mioyo yao yote. Jambo hili halingewafanya wawe waovu. Ndipo Yesu akawaambia, "Basi alichokung'anisha Mungu, mwanadamu asikitenganishe" (Marko 10:9). Alitaka kuwaonyesha Mafarisayo kwamba ni mapenzi ya Mungu kwa mwanamume na mwanamke kuishi pamoja jinsi ilivyoandikwa katika Mwanzo 2:24. Aliwaambia pia kwamba talaka ni dhambi. "...Kila mtu atakayemwacha mkewe na kuoa mwingine azini juu yake; na mke akimwacha mumewe na kuolewa na mtu mwingine, azini" (Marko 10:11-12). Biblia inendelea kutwambia kwamba wanfauni walishangaa walipomsika Yesu akizungumzia juu ya usafi, na ndoa kwa sababu walikuwa

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. Wabeshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi" (Waefeso 6:1-2).

KUSOMA SOMO

UTANGULIZI

Mtu dhauti atapata nguvu kwa kumtii na kumwamini Mungu, na kwa kuziamini ahadi zake. Kutofaulu kwao kunaweza kuwa ushindi. Walio kata tamaa wanaweza kuanza kuwa na tumaini. Lakini wale ambao hawamtii Mungu hawana tumaini la uzima.

Kutotii huleta majuto, huzuni na taabu. Mfano mzuri unapatikana katika Biblia, 1 Samueli 2:12-36. Inaeleza juu ya Eli na wanawe. Eli alikuwa kuhani wa Bwana, na aliishi katika hema ya Bwana. Wanawe walikuwa pia makuhani ambao walimtolea Mungu dhabinu (sadaka) katika hema lililokuwa Shilo. Wana wa Eli walifanya dhambi mbele za Mungu, wala hawakusikiliza maonyo ya baba yao juu ya kutenda maovu katika nyumba ya Mungu. Hawakufuata kanuni za makuhani kuhusu mapato yao kutoka kwa watu. Wana wa Eli walikula ile sehemu nono ya wanyama waliouwiwa kutolewa dhabinu wakati Waisraeli walipomtolea Mungu dhabinu zao. Hawakuliheshimu dhabinu ya Bwana.

Eli, ambaye kwa sasa alikuwa amezeeka alisikia malalamiko ya watu waliocenda kutoa sadaka zao huko Shilo. Wanawe walikuwa wakizini na wanawake walioliana kazi katika lango la hema.

Eli aliwaonya wanawe na kuwakanya waache maovu waliyokuwa wakifanya, lakini hawakumsikiliza baba yao. Kwa hivyo Bwana aliamua kuwaua. Mungu alimwambia Eli kupitia kwa nabii kwamba ataondoa uongozi wa ukuhani kutoka kwa jamaa yake. Jamaa yake wangukuwa daima maskini, na

Baba kama kichwa cha jamaa, anapaswa kuchukua jukumu la kuongoza ibada ya jamaa. Lakini mama anaweza kuongoza kama baba hataki. La siyo, Mkristo ye yote anaweza kuongoza. Huu ndio wakati ambapo jamaa yaweza kujifunza Neno la Mungu, kukua katika imani na kuwa karibu na Mungu. Tunapaswa kukumbuka pia baraka za ibada ya kanisa ambapo wazazi wanaweza kuwaambia jamaa yao wakae pamoja. Kisha wazazi wanaweza kuhakikisha kwamba watoto hawawasumbui watu wengine. Wanajifunza pamoja habari za Mungu.

KAZI YA KUFANYA

1. Mwombe Mungu akupe ujasiri wa kuanzisha ibada ya jamaa na kwamba utaiendeleza hata kwa nyumba yako mwenyewe.
2. Andika jinsi mnavyobarikiwa na ibada ya jamaa, kama mnaifanya nyumbani kwenu.
3. Kama hamna ibada ya jamaa nyumbani kwenu, zungumzana na wazazi wako kuhusu kuianzisha.

SURA YA KUMI NA MOJA

AMRI ZA MUNGU KWA MTOTO

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba watoto wanapaswa kuwatii wazazi wao, na wazima wanapaswa kuwaheshimu wazazi wao.

SOMO KUTOKA: Kutoka 20:12; Waefeso 6:1-3; Mathayo 19:19; Warumi 5:19

VIFUNGU VYA LEO: Waefeso 6:1-3; Luka 2:51; Wakolosai 3:20; Mithali 13:1; 1 Petro 1:14

wamejifunza sheria ya Musa. Mungu alitaka watu waelewe kwamba anataka mume na mke waishi pamoja milele. Wangetenganishwa na kifo tu.

MAFUNZO YA SURA HII KWANGU

Siku zote mpango wa Mungu kwa mwanadamu ni mwema, lakini mwanadamu amekuwa akitaka kuishi bila Mungu. Nia hii huleta shida. Mungu alimwumba mwanamume mmoja na mke mmoja kuishi pamoja jinsi ilivyoandikwa katika Mwanzo 1:27, lakini tunaona kwamba mwanadamu alibadili mpango wa Mungu kwa kuwaoa wake wengi.

Mungu alipanga pia kwamba mume na mke wapandane, na waheshimiane. Lakini baadhi ya watu hugombana na kutaka wafanye wapendavyo badala ya kusikilizana. Kisha hupeana talaka kwa sababu hawana upendo ambao Mungu alinuia wawe nao. Biblia inatufundisha kwamba si vyema kuachana. Katika 1 Wakorintho 7:2-3 kila mwanamume amcambiwa kwamba awe na mkewe binafsi. Musa aliwaruhusu watu kuachana, lakini hiyo haikuwa nia ya Mungu. Musa aliwaruhusu kwa sababu ya hali ya kiroho ya kutotosheka kwa mwanadamu. Waume na wake Wakristo wanapaswa kuishi pamoja. Wakristo wanapaswa kuwa tayari kusamehe kila wakati. Soma Mathayo 18:21-35. Tunaweza kumshawishi mtu huyo tunapomsamehe na pia tutakuwa na hazina mbinguni.

Wakati mume na mke wanapochana, yule anayeo tena huwa amezini. Hii inaonyesha kwamba hakuna aliye mkuu kati ya mume na mke. Wote ni sawa mbele za Mungu. Mume ni kichwa cha mke jinsi Kristo alivyo kichwa cha kanisa. (Waefeso 5:21-23) Yeye si mtumwa wala mali ya mume. Yeye amesimama kando ya mumewe, wakiwa sawa katika Kristo kwa imani na heshima. Biblia inafundisha kwamba, "...Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninvi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu" (Wagalatia 3:28).

Mpango wa Mungu ni ule ule jana, leo na hata milele.

KAZI YA KUFANYA

1. Je! watu wakichana hupata shida gani? Ziandike kwenye karatasi.
2. Je! Wakristo wanapaswa kuwatendeaje watu ambao wameachana? Je! Kanisa lako litawafanya nini?
3. Ombea ndoa yako. Mwombe Mungu akusaidie kuamua kwamba talaka siyo suluhisho shida zikitoka katika ndoa yako. Jitoe kusuluhisha shida zako kwa kufuata mwongozo wake.

SURA YA NNE

MAISHA YA MKRISTO NYUMBANI

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba ni lazima nionyeshe kwanza Ukristo wangu nyumbani.

SOMO KUTOKA: Yakobo 1:19-20; Wakolosai 3:8, 12-13, 19-20; Zaburi 19:14; Yohana 13:34; Waefeso 4:15

VIFUNGU VYA LEO: Yakobo 1:19-20; Wakolosai 3:8, 12-13, 19-20; Zaburi 19:14; Yohana 13:34; Waefeso 4:15

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Maneno ya kinywa changu, Na mavazo ya moyo wangu, Yapaie kibali mbele zako, Ee Bwana, Mwamba wangu na Mwokozi wangu" (Zaburi 19:14).

KUSOMA SOMO

UTANGULIZI

Yohana alikuwa akienda nyumbani kutoka kanisani baada ya mazoezi ya kwaya. Alitegemewa sana katika kwaya yao na kila

nyumba za Wakristo picha za arusi na kalenda. Kumbuka kwamba picha ni njia nzuri ya kuwafundisha watoto.

Matendo 2:46-47 inatwambia kwamba waamini walishiriki chakula manyumbani mwao, wakila kwa furaha na roho ya ukarimu, wakintukuza Mungu na kufurahia baraka za watu wengine. Ni kwa njia ya ibada ya jamaa ambapo wazazi na watoto wanaweza kufanya mapenzi ya Mungu kwa pamoja.

MAFUNZO YA SURA HII KWANGU

Wazazi wengi wa kizazi cha leo wamepuuza wajibu wao wa kukusanyika pamoja na kuabudu, kuwaongoza na kuwashauri. Vijana wa siku hizi wanapaswa kujishughulisha ili wakue Kikristo. Wengine wanaweza kuuiliza, "Je! itakuje ikiwa hatuna ibada ya Kikristo nyumbani kwetu." Itakuwa wajibu wako kuomba na kuanzisha. Jadiliana na wazazi wako jinsi unavyofikiria kuanzisha ibada ya jamaa. Wakikubali, basi pageni saa ambayo itafaa wakati kila mmoja atakuwa yuko nyumbani na ashiriki. Ibad hiyo inapaswa kuwa na maombi, nyimbo zinazofaa waliohudhuria, kusoma Biblia, kuelezea maandiko, na kuyalinganisha na maisha ya kisasa. Ni vizuri kujifunza kukariri vifungu vya Biblia. Mwishowe, mmoja anaweza kuomba na wengine wanarudia. Unapoomba mshtukuru Mungu na umwombe aongoze mahitaji miyo nayo. Waombeeni watu wengine wenye mahitaji, na umwombe Mungu azidi kuitia nguvu ibada ya jamaa yako.

Unapaswa kuomba pingamizi zo zote ambazo zitawazuia kuanzisha ibada ya jamaa. Inaweza kuchukua muda mrefu au muda mfupi kujibiwa maombi yako. Muda wa majibu ya maombi si kitu. Unapaswa kuwa mwaminifu katika ibada yenu. Uwaiti na kunyenyekea wazazi wako, naye Mungu atajibu maombi yako kwa wakati wake.

Ukifikiria vizuri katika ujana wako, unaweza kukumbuka mambo uliyosikia ukiwa na umri wa miaka mitano hadi kumi. Kwa hivyo unapaswa kuwafundisha watoto kuwa Mungu anawapenda, nao wampenda Mungu. Wanaweza kujifunza jinsi ya kuomba na kufanya kazi za kanisa wakati wa ibada ya jamaa.

Watoto wanaweza kukariri kwa haraka sala iliyoko katika Mathayo 6:9-13. Ni lazima uendelee kuwakumbusha Mungu anavyowatarajia wafanye tangu utotoni hadi katika utu uzima. Ni lazima wajue na waelewe kwamba kila kitu wanachooona kilimbwa na Mungu. Ufunuo 14:7b inasema, "...Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji." Mnapotembea waonyeshe mimea, ndege na wanyama kama viumbe vya Mungu. Wanapokula wafanye wajue kwamba Mungu ni mwema na mpole na ndiye aliyeumba chakula chote walicho nacho. Wakumbushe kwamba Mungu husikiliza wakati watu wanaposema naye kwa njia ya maombi. Wajue kuwa anatumiza mahitaji yetu.

Watoto wanapaswa kufundishwa jinsi ya kushirikiana na wengine wakati wa ibada ya jamaa na wanapaswa kunyamaza wakiwa kanisani ili tu kama wanatumia sauti zao kuabudu. Kumshukuru Mungu wakati wa mahitaji na wakati unaposaidiwa ni njia moja wapoya kukua kwa Mkristo. Jambo lingine ni kuwaombea wenzako wote, hata maadui. Ni lazima mtoto ajue jinsi ya kuwaamini wazazi na Mungu na kuwa mwema jinsi inavyompasa. Mtoto huyo anapaswa pia kujifunza kushiriki na wenzake, awe na kitu kikubwa au kidogo. Mungu ametuamuru tutoe na tuwe wakarimu kwa wengine.

Kumbukumbu la Torati 6:9 inasema kwamba waandike amri hizo kwenye vizingiti vya nyumba na milango. Mchungaji mmoja alisema kwamba hukosi kuona picha ya Aga Kahn katika nyumba za wafuasi wake, lakini utakuta kwenye kuta za

mwimbaji alimbeshimu. Lakini alikuwa na huzuni hata baada ya kufurahiwa na wana kwaya. Mwenyewe aliona ni afadhali abaki kanisani ambako kila mmoja alitamani uwezo na wema wake.

Alikumbuka kilichofanyika kabla ya kwenda kanisani. Mama yake alimwambia aende kutafuta kuni kabla ya kuondoka. Lakini alimjibu mama yake kwa ukaidi akisema, "Sitafanya hivyo!" Mama yake alimwambia kwamba atamshitaki kwa baba yake.

Yohana alijua kwamba baba yake atamwadhibu kwa tendo alilofanya. Hakuwa na nia ya kutubu. Alifikiria jinsi atakavyokataa adhabu ya baba yake. Hata alifikiria vile atakavyo wapiga ndugu na dada zake wadogo baada ya kuadhibiwa. Hii ndiyo sababu hakufurahia kwenda nyumbani.

MAELEZO

Mmojawapo ya shida ya Yohana ilikuwa hasira. Aliwakasirikia wazazi wake na hata yeye mwenyewe. Tukiwa na hasira hatuwezi kusikiliza vizuri wala kuwasiliana vizuri. Kitabu cha Yakobo kinafundisha hatua muhimu zifuatazo ambazo zaweza kutusaidia. (Yakobo 1:19-20)

Uwe mwepesi wa kusikia. Mungu ametupatia masikio ya kutusaidia tunaposhirikiana. Kwa masikio yetu tunasikia maneno mazuri au maneno ya kutisha. Tunapaswa kuwa wepesi wa kusikia. Ni wajibu wetu kutofautisha lililo jema au baya kwa kusikiliza.

Usiwe mwepesi wa kusema. Tumezoea kusema mara baada ya kusikia. Biblia inatuonya kwamba tusiwe wasemaji kwa kila jambo tunalosikia. Ni lazima tufikirie kwa makini kuhusu yale tuliyoikia ili tuwe na uhakika tunapolisema, kwa sababu tunaweza kuwakasirisha wengine kwa usemi.

Msiwe wepesi wa hasira. Tunaweza kukasirishwa na baadhi ya yale tunayosikia. Hatuwezi kujizua tukiwa na hasira. Tunaweza kuamua kupipiza kisasi, wakati Biblia inakataza jambo hili. Tunaweza kuamua kupigana, na tumeambiwa tuwe wapole. Yakobo 1:20 inasema, "...hasira ya mwanadamu haicendi haki ya Mungu."

Yohana katika Utangulizi asingekuwa na uhusiano mbaya na wazazi wake kama angeyafuata maonyo ya Biblia.

Tunatarajiwa kuishi maisha mapya tunapokuwa Wakristo, Maisha na mwenendo wa Mkristo vinajulikana hata na watu wasio Wakristo. Wanataka kuishi hivyo, lakini hawawezi bila ya kuwa na Yesu Kristo maishani mwao.

Kuna baadhi ya mambo ambayo mtu anapaswa kuacha baada ya kuwa Mkristo. Soma Wakolosai 3:8. Je! kulingana na kifungu hiki ulimi wa Mkristo unapaswa uweje? Mambo haya hasira, ghadhabu, uovu, matukano na matusi hayapaswi kutoka vinywani mwa Wakristo. Bali Mkristo anapaswa kuishi jinsi inavyoelezwa katika kitabu hicho hicho, Wakolosai 3:12-13.

Mkristo anapaswa kujua kwamba yeye ni mteule, mtakaifu na anayependwa na Mungu. Soma kifungu cha 12. Hii itamsaidia kuishi kila siku kwa sababu atakuwa na uhakika po pote alipo. Kisha matokeo yake yatakuwa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole na uvumilivu jinsi tunavyoambiwa katika kifungu hicho.

Mkristo anapaswa kujua pia kwamba watu ni tofauti. Kuishi na wengine kunahitaji mambo mawili:

1. Ustahimilivu: Ni lazima hii iwe tabia ya Mkristo kwa watu wengine wanaofanya mambo tofauti au wanaopinga anayoyafanya na kuyasema. Sisi Wakristo tunapaswa kuwahurumia wengine hata adui zetu.

Wazazi hao hawakutumia Biblia, lakini walijua wajibu wao wa kuwafundisha watoto wao. Inapaswa kuwa aombi na mtindo wetu kuendeleza mtindo wa zamani wa ibada ya jamaa na kuifanya iwe ibada ya jamaa ya kibiblia ambayo jamaa hukutanika kusoma Neno la Mungu.

MAELEZO

Katika Kumbukumbu la Torati 6:4-9, Waisraeli waliambiwa wampende Mungu kwa moyo, roho na nguvu zao zote. Waliambiwa wasisahau amri walizopewa. Kifungu cha 7 kinasema kwamba walipaswa kuwafundisha watoto wao amri hizi, kuzirudia wakiwa nyumbani na po pote walipo, hata walipokuwa wakipumzika au wakifanya kazi. Walipaswa kufunga amri hizi kwenye mikono yao na waziwae kwenye paja la uso kama ukumbusho. Walipaswa kuziandika kwenye vizingiti vya nyumba zao na kwenye mliango.

Watu wengi wanaosoma vifungu hivi hawaviii maanani! Je! kwa nini? Wanafikiri kwamba wanaelewa vizuri mahitaji ya watoto wao kuliko Mungu. Hii ndiyo sababu wamepuuza wajibu wao wa kuwafundisha watoto hata jinsi ya kumwabudu Mungu. Mithali 22:6 inasema kwamba wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao jinsi ya kuishi, nao hawasahanu milele.

Ibada ya jamaa ni wakati muhimu kwa Wakristo, hasa wazazi na watoto. Watoto watapata nafasi ya kujifunza kutoka kwa wazazi wao yale ambayo Mungu anataka wafanye wanapokutanika pamoja. Baadhi ya watu hufikiri kwamba watoto wadogo hawawezi kujifunza mambo, kwa hivyo wanawona kujifunza ni kupoteza wakati. Ni lazima waelewe kwamba watoto hujifunza vizuri ikiwa wanafundishwa kwa mtindo mzuri.

SURA YA KUMI

IBADA YA JAMAA

KUSUDI LA SOMO HILI: Ni lazima nijifunze jinsi jamaa yangu inavyopaswa kumwabudu Mungu pamoja.

SOMO KUTOKA: Kumbukumbu la Torati 6:4-9; Matendo 2:46-47; Ufunuo 14:7

VIFUNGU VYA LEO: Kumbukumbu la Torati 6:4-9; Matendo 2:46-47; Ufunuo 14:7

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msjudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji" (Ufunuo 14:7).

KUSOMA SOMO

UTANGULIZI

Neno, ibada, ni pana sana katika Biblia, lakini katika Biblia nzima linatumika kwa maana ya "kutumika." Unapofikiria juu ya ibada ya jamaa unapaswa kukumbuka kwamba dhambi na Shetani ni maadui wa Wakristo na wasio Wakristo ulimwenguni kote, Shetani hataki jamaa yako ifanye ibada. Atajaribu kuwavunja moyo katika kila jambo, lakini Yesu atakusaidia na utajifunza kumwabudu Mungu kwa roho na kweli. (Yohana 4:24)

Wazo la ibada ya jamaa si jambo geni kwa Waafrika. Wazazi walikuwa wakiwafunza watoto wao kila siku baada ya chakula: Waliwashauri jinsi ya kukabiliana na maisha yao ya baadaye. Wazazi walimfahamu Mungu kama Mwumba wa wanadamu na aliyewaamuru wamtii. Akina baba waliwafunza wavulana na akina mama waliwafunza wasichana. Waliwafundisha jinsi ya kukubali wajibu kwa kutofautisha mema na mabaya.

2. Msamaha: Ni muhimu kwa Wakristo kuwasamehe wale waliofanya au waliosema mabaya juu yao. Lakini haiishii hapo tu. Tunapaswa pia kusahau kwamba jambo kama hilo limetokea na tuwe tayari kumkubali mtu huyo kama kwamba hakujafanyika cho chote. Unapaswa kuwasamehe wengine ikiwa Mungu amekusamehe (kifungu cha 13).

Shida ya Yohana ilikuwa kwamba alijifanya mzuri nje na akawa mtundu akiwa nyumbani kwao. Mfume Paulo alisisitiza uelewano katika jamaa. Itakuwa rahisi kutii, kupenda na kutochokozana katika jamaa kama kila mmoja atatekeleza vyema wajibu wake wa Kikristo. (vifungu 18-20)

Upendo na umoja ndiyo ishara kuu ya ushirika wa Kikristo. Yesu Kristo alifanya amri zote kuwa moja: "...Mpendane..." (Yohana 13:34). Upendo huu unapaswa kuanzia nyumbani. Huwezi kuwapenda watu wengine kama hupendi jamaa yako. Kama una jamaa ambayo haifuati mfano huu, basi waombe. Mungu atawabadilisha. Ana uwezo kufanya mwiujiza.

Pengine utafikiria au kupanga aina ya jamaa unayoitegemea kwa kujifunza kutoka kwa jamaa yako. Usirudie makosa yale yale unayoyaona katika jamaa yako. Ni lazima uwe tayari kuanzisha jamaa bora.

Pengine unafikiria kwamba ni vigumu kufanya hivyo, lakini Kifungu cha Kukumbuka chetu ni muhimu. Tumwombe Mungu aongoze fikira, matendo na maneno yetu. Tutaonyesha kukomaa tunaposema kwa upendo. Soma Waefeso 4:15. Yote haya yanapaswa kuanzia nyumbani.

MAFUNZO YA SURA HII KWANGU

Tunapaswa kujifikiria sisi wenyewe baada ya kusoma habari ya Yohana. Pengine utafikiria kwamba wazazi wa Yohana walikuwa wakatii au Yohana alikosea kwa matendo yake.

Hata kama wazazi wako wamekosea, ni wajibu wako kuwatii, isipokuwa kama maagizo yao hayaambatani na mafundisho ya Bwana Mungu. Waombe kila siku na uwaonyeshe upendo, upole na heshima. Unapaswa kuwasamehe kila wakati iwapo wamekukosea. Wazazi wako watafurahi ikiwa utajifunza kuwaomba msamaha unapokosa.

Ukiwa Mkristo unapaswa kuwa baraka kwa jamaa yako. Utajifunza jinsi ya kutunza jamaa yako baadaye kwa kuwasaidia kwanza wadogo zako. Utawafanya wamwamini Bwana kama hawajamwamini ikiwa utakuwa mpole na mnyenyekevu kwao.

KAZI YA KUFANYA

1. Hebu mfikirie Yohana na tabia yake. Tafuta udhaifu na uwezo alokuwa nao.
2. Ifikirie jamaa yako. Andika orodha ya mambo mema unayozaona nyumbani kweni. Andika orodha ya mambo yale ambayo ungependa yabadilishwe. Ombea udhaifu ulioko na umshukuru Mungu kwa yote mema yaliyoko nyumbani kweni.
3. Je! ungependa kuwa mume au mke wa aina gani, unapofikiria nyumba (jamaa) utakayokuwa nayo siku zijazo? Je! ungependa kuwa mzazi wa aina gani? Anza kuombea jamaa unayotaka kuwa nayo.

Kuna thibitisho la kutosha katika makansa ya siku hizi kwamba wazazi wamepuuza wajibu wao wa kuwaonya watoto. Watoto hufanya kekele na kucheza, kuingia nakutoka nje, na kucheke na kuzungumza na wenzao. Je! kwa nini? Kwa sababu watoto hawafundishwi umuhimu wa kuthulia na kuwa na heshima kanisani. Si rahisi kuwasimamia watoto, lakini ni lazima unyeshe upendo na kumwonya kila mtoto.

Ni lazima wazazi wajihadhari na majadiliano mbele ya watoto wao. Hawana uwezo au hitaji la kukata mashauri juu ya shida nyingi.

Hakikisha kwamba watoto wako wanawajua watu wa ukoo wenu na marafiki. Wafundishe kuwakeshimu babu na nyanja, na wazee wengine. Ni vigumu kuonyesha upendo na kuwaonya watoto, lakini yote yanawezekana, kupitia kwa Mungu ambaye ni nguvu na hekima yako. Wakati mwingine upendo na maonyo huonekana kama haviwezekani, lakini mzazi anapomwonyesha mwanawe upendo, mtoto huyo hutaka kumtii ili kudumisha upendo huo.

KAZI YA KUFANYA

1. Mwombe Mungu akuonyeshe mambo katika maisha yako unayostahili kujirudi.
2. Je! utaamua kufanya nini kuhusu kuonya na kuirudi nyumba yako?
3. Je! unafikiri ni kwa nini Mungu aliwapa wazazi amri hii?

ukamilifu. Mungu anamtarajia kila mzazi kuchukua wajibu huu muhimu wa kuwaonya na kuwarudi watoto wao. La sivyo, wazazi watalumiwa kwa makosa ya watoto wao. Mtoto mwenye wajibu atatoka katika jamaa ambayo ina upendo na maonyo. Ni amri kutoka kwa Mungu. Ichukue na utumie.

MAFUNZO YA SURA HII KWANGU

Je! unaweza kufikiria jinsi utakavyotimiza wajibu wako wa kuwaonya watoto wako?

Ni lazima uhakikishe kwamba uhusiano wako na Mungu na watu wengine ni mwema kabla ya kuanza kumsaidia mwingine abadili tabia yake. Hivyo basi, Mungu atakusaidia utanye anayokutarajia. Kuonya na kurudi sio tu kumwadhibu mtoto kwa kukosa. Ni kumfundisha kutimiza wajibu wake akiwa nyumbani, shuleni na katika uhusiano wote wa maisha yake. Maonyo na marudi husaidia kurekebisha nia na tabia. Mtoto hujifunza jinsi ya kuitikia mambo maishani kwa kuonywa.

Wazazi wanao wajibu wa kuwafundisha watoto wao mambo muhimu ili waweze kujitunza wenyewe na nyumba zao. Wasichana wengi hufikia wakati wa kuolewa hali hawajui kupika wala kusafisha nyumba. Wazazi husema kwamba wameshindwa kuwafundisha kwa sababu mfanya kazi hufanya kazi zote za nyumbani. Je! msichana kama huyu atakuwa mke au mama wa aina gani?

Wavulana hukua na kuwa wazima bila kujua wajibu wa baba. Kisa ni kwamba baba zao huja nyumbani usiku na hawana nafasi ya kuzungumzana na vijana wao. Je! ni nani anayepaswa kulaumiwa?

Ni lazima watoto waonywe na kurudiwa katika kila kazi ya nyumbani. Si jambo la kuamua kuwaonya watoto. Ni amri kutoka kwa Mungu.

SURA YA TANO

AMRI ZA MUNGU KWA MUME

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza matarajio ya Mungu kwa mume.

SOMO KUTOKA: Waefeso 5:25, 28, 33; Wakolosai 3:19; 1 Wakorintho 11:3 VIFUNGU VYA LEO: Waefeso 5:25, 28, 33; Wakolosai 3:19; 1 Wakorintho 11:3

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake" (Waefeso 5:25).

KUSOMA SOMO

UTANGULIZI

Maria na mchumba wake, Yohana, walianua kuoana baada ya kumaliza shule. Wote walifurahia sana maisha yao mapya. Alizaa mtoto wa kike katika mwaka wa pili wa ndoa yao. Jambo hili lilifanya uhusiano wao kuwa wa ajabu. Upendo wao ulikuwa siku baada ya siku jinsi walivyozidi kuvumbua mambo pamoja.

Waliendelea vizuri lakini mambo yalibadilika wakati walipopata msichana wa sita. Yohana alibadilika kabisa. "Nimechoka kuona watoto wa kike mwaka," akasema. Alianza kutembea siku za Jumamosi na Jumapili na kurudi nyumbani usiku. Jamaa yake hawakuwa na pesa za kutosha kununua chakula na inaaminika kwamba alianza kunywa pombe. Yohana angejifunza mengi kwa kusoma Neno la Mungu na kuona wajibu wa kila mwanamume. Hebu sasa tujifunze mambo haya.

MAELEZO

Mfungu amewamuru waume wawapende wake zao jinsi Yesu alivyolipenda kanisa na kujitoa kwa ajili yake.

Wanaume wanapaswa kuwapenda wake zao jinsi wanavyoipenda mili yao. Mwanamume anayempenda mke wake anajipenda mwenyewe. Hakuna mtu anayechukua mwili wake. Bali huutunza vizuri jinsi awezayo. Sehemu moja inapoumia mwili wote hudhurika. Ndiyo maana tunaitunza mili yetu. Tunaavaa nguo nzuri na kula chakula bora. Tunataka kuka na usalama wa maisha yetu. Tunakaa mahali penye, joto na kinga ili tusinyeshewa wakati wa mvua. Tunahitaji kupumzika vya kutuoshia, hasa baada ya kazi ngumu. Paulo amesema katika Wakolosai 3:19 kwamba waume wanapaswa kuwapenda wake zao, wala wasiwe wakali kwao. Kwa hivyo, tunapaswa kujua na kuelewa kwamba Mungu hawasilhi waume wawapende wake zao, bali anawaamuru kuwapenda na kuwatunza. Neno hili, upendo, jinsi liliyotumiwa, maana yake ni kutunza na kushughulikia masilahi ya mtu mwingine bila kujali gharama. Waume ni vichwa vya jamaa zao, na wanapaswa kuwapenda wake zao jinsi wanavyoipenda. Neno hili, kichwa, lina maana ya kuonyesha mawasiliano mema katika jamaa. Kisha kila mmoja huelewa wajibu wake na kuitikia ipasavyo.

Jamaa si jamaa kama hakuna makubaliano kuhusu kutimiza malengo yao kwa pamoja. Waume mara nyingi hukataa kutumia wakati wao kuzungumzia mambo ya jamaa zao. Hawawezi kujadili shida zao ili udhaifu na uwezo wao usjulikane. Waume na wake wanapaswa kujadiliana shida zao na kufanya mabadiliko ambayo yataendeleva maisha yao na wawe na jamaa (nyumba) bora. Jamaa inapaswa kushirikiana kama kitu kimoja. Mke hapaswi kuchukuliwa kama mali ya mume, bali kama msaidizi wake. Anapaswa kuwa rafiki

Bwana humuonya mtu ye yote anayempenda na humwadhibu mtu ye yote anayemkubali kama mwanawe. Viiyo hivyo wazazi nao huwaadhibu watoto wao, nao huendelea kuwaheshimu. Wale wanaoadhibiwa watauma tuzo la maisha ya haki wakati ujao.

Unapowaangalia vijana wa siku hizi unaweza kuona kwamba kuna shida nyingi mbele yao. Nyingi za hizo hutoka sababu wazazi wao hawapendi kuwarudi watoto wao wakiwa wadogo. Ni lazima uwafundishe watoto wako tangu utotoni ikiwa unataka wawe wema, wapole, wawumilivu, wenye kutosheka, waaminifu na wasio na choyo. Unaweza kusaidia kuyanda maisha ya mtoto wako.

Mithali 13:24 inatonyesha kwamba ikiwa hatuwaadhibu watoto wetu basi hatuwapendi. Ni lazima tuwaonyeshe yaliyo ya haki kama tunawapenda. Watoto wanapaswa kuonywa na kurudiwa. Kwa sababu huwa wanakosa bila kujua. Uapaswa kuwachapa, lakini ni vizuri kuzungumza nao kuhusu shida hiyo. Watalewa yale ambayo huyapendi na kwa nini ni mabaya.

Baadhi ya wazazi hufikiri kwamba shule zipo ili kuwaadhibu watoto wao kwa niaba yao. Wakitunata wazo hili, basi wanakosa kutii amri ya Mungu kwa wazazi kuvala na kuwarudi watoto wao. Ni lazima uchukue wajibu wako kama mzazi ili kuhakikisha kwamba mtoto wako atakuwa na tabia nzuri. Tunaambiwa katika Mithali 29:15-17 kwamba kuonya na kumtudi mtoto ni vizuri. Inaendelea kusema kwamba mtoto aliyechuliwa humwaibisha mamaye. Kitungu cha 16 kinatukumbusha kwamba masi huongezeka wakati watu waovu wanapopata mamlaka. Bali mwenye haki ataishi apate kuona maanguko yao.

Katika kifungu cha 17, wazazi wamechumiwa kuonya watoto wao ili wapate kujivunia. Kwa kweli, mtoto ataonekana kuwa anastahili na ana wajibu ikiwa mzazi amatahuri vizuri kwa

KUSOMA SOMO

UTANGULIZI

Stefano na Martha ni wazazi waliomlea mwanao pekee wakati wa shida. Kitu cha pekee walichokuwa nacho ni shamba na ng'ombe wawili. Kijana huyu alipotimiza umri wa miaka saba, aliachwa kufanya cho chote alichotaka. Wazazi wake hawakujishughulisha na kumfundisha kutofautisha katika mema na mabaya.

Mambo yalianza kubadilika siku baada ya siku hadi siku moja kijana huyu akaamua kuchukua kitu cha mtu mwingine. Kijana huyu alianza na vitu kama sahani, sufuria na kuku. Kisha zikawa mbuzi, kondoo na ng'ombe. Baba na mama yake walipokea vitu hivyo kila wakati alipovileta nyumbani. Walikuwa wakimhimiza mtoto wao kwa kupokea vitu alivyowaletea.

Kijana huyu aliwaibia sana majirani mpaka wakaanza kulalamika. Kisha siku moja aliiba ng'ombe ya mzee wa kijiji. Mzee huyu aliwatuma watu watafute mwizi huyo. Muda si muda, kijana huyu alipatikana na akashikwa. Alimsikia mtu akisema "Ngombe yuko hapa, tumempata mwizi." Hakuweza kutoroka. Alishikwa na akapelekwa gerezeni.

Je! shida ya kijana huyu ilikuwa nini? Je! unafikiri angekuwa na tabia tofauti kama wazazi wake wangemfundisha mambo tofauti? Je! utafanya uamuzi gani ambao utakusaidia kuzuia jambo kama hili kutokea katika jamaa yako? Je! Biblia inasema nini kuhusu jambo hili? Hebu tujifunze habari hiyo.

MAELEZO

Biblia inatukumbusha kwamba Mungu hasahau kuwatia moyo watoto wake, na ni wajibu wetu kusikiliza au kutosikiliza. (Waebrania 12:5-11)

ambaye anaweza kuzungumza na mumewe kuhusu shida na matatizo ya maisha. Inasemekana kwamba waume wengi hujishughulisha na shida zao wenyewe na kuzitatusa kisiri. Hiyo si njia nzuri ya kukabili hali hii. Wake wanapaswa kuhusika.

Tendo la kuwalea watoto ni wajibu ambao waume wengi huukwepa. Wamejitenga na hata hawajali. Wanapaswa kuelewa kwamba watoto wenye tabia nzuri huwaletea sifa wazazi wao. Malezi na mafunzo ya watoto hayapaswi kuachiwa akina mama tu.

Maneno ambayo mume hutumia kuomba au kumwambia mke kitu ni ya muhimu sana. Kuna methali inayosema kwamba, "Maneno mazuri humtoa nyoka pangoni." Waume wanapaswa kujua kwamba maneno makali wanayotumia kusema na wake zao huleta chuki kati yao. (Waefero 4:29) Mke hawezi kumwambia mumewe woga wake au jinsi anavyofikiria kutatua shida fulani katika jamaa yao kama mumewe atamjibu kwa ukali. Mume na mke ni watu wawili tofauti wenye mawazo tofauti. Lakini wanapaswa wajifunze jinsi ya kuelewana. Mume anapaswa kumwonyesha upendo mwingi mkewe. Anapaswa kumwombea kila wakati. Mume anapaswa kuchukua wajibu wa kumwongoza mke wake ajitoe kwa Bwana jinsi Kristo alivyolifanyia kanisa, kama mke hawezi mwenyewe au kama si Mkristo.

MAFUNZO YA SURA HII KWANGU

Hitaji muhimu la kupendana ni la mtu kujitoe kwa Yesu Kristo awe Bwana. Huu ndiyo msingi wa kujitoe. Kisha tunaweza kumruhusu atuongoze anavyotaka. Ni vigumu watu wasio Wakristo kuwaonyesha wenzao wao upendo. Wanaonekana kuwa hawajali, na uchoyo wao huleta kutoelewana.

Hata hivyo, Bwana atakungoza kuamua sasa juu ya nyumba (jamaa) yako ya baadaye. Je! unatarajia kuwa na nyumba ya ajabu na yenye amani? Basi ni lazima uwe tayari kupenda, kutunza na kujitoa kwa mume au mke ambaye utamwoa. Mke ni mke kwa mume hata kama atazaa wasichana tu au hata kama hatazaa. Kutozaa wavulana si sababu ya kumwacha au kuoa mwingine. Mungu anajua yanayotufaa sisi, na ni lazima tuamini uamuzi wake. Mapenzi yake si mapenzi yetu, lakini tunapaswa kukubali.

Mungu anatarajia waume kuwapenda wake zao na kuwatunza jinsi wanavyoiondea mili yao wenyewe. Nia kama hii itakusaidia kujenga jamaa yenye furaha - ile ambayo Mungu alikupangia uwe nayo ulimwengu. Mungu huheshimiwa katika nyumba ya Kikristo ambayo ina mume na mke wanaopanga mambo pamoja na kuyafanya. Hii hutoka kukiwa na mawasiliano mema katika jamaa. Mwombe Mungu akusaidie kufanya uamuzi wa kufaa maisha yako yajayo. Mwombe kuonyeshe anayotaka ufanye.

KAZI YA KUFANYA

1. Sema Kifungu cha Kukumbuka kila asubuhi kabla ya kutoka kitandani.
2. Je! huwa unaelewa nini wakati neno, upendo, linapotajwa?
3. Andika baadhi ya mambo uliyojifunza kwamba mume Mkristo anapaswa kufanya. Je! nini chanzo za kuwepo waume wasiojali?
4. Je! unapangaje kukua jamaa yenye furaha?

kisingizio kwamba hawakufundishwa cho chote. Kanisa liko tayari kuwashauri wazazi na watoto kama jamaa. Biblia ina mafundisho mengi kuhusu mtoto anavyopaswa kufundishwa. Mwombe Mungu akutayarisha kuwa mzazi mwema kama anavyokutajia. Amua leo kwamba utakuwa na wajibu kwa watoto wako kuwafundisha wanayopaswa kujua. Tumia nafasi ya wakati ulio nao kwa kusoma na kuandika mambo ambayo yatakusaidia kuwa mzazi mwema wakati wako utakapofika.

Mwombe Mungu mweza yote akujaze na hekima.

KAZI YA KUFANYA

1. Mwombe Mungu akutayarisha kuwa mzazi mwema wakati wako utakapofika.
2. Je! kwa nini wazazi wa siku hizi wamepuuza wajibu wao wa kuwafundisha watoto? Je! utafanya nini kuhusu jambo hili?

SURA YA TISA

JE! NI NANI ANAYESTAHILI KUWALEA NA KUWARUDI WATOTO?

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba wazazi wanao wajibu wa kuwalea na kuwarudi watoto wao.

SOMO KUTOKA: Waebrania 12:5-11; Mithali 3:11-12; 13:24; 29:15-17

VIFUNGU VYA LEO: Waebrania 12:5-11; Mithali 3:11-12; 13:24; 29:15-17

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Yeye asiyetumia fimbo yake humchukia mwanawe; Bali yeye ampendaye humrudi mapema" (Mithali 13:24).

Ni lazima wazazi watake watoto wajifunze nguvu za maombi. Watoto watajifunza kumwomba Mungu wakiwa na shida kama watawaona wazazi wao wakiombea shida walizo nazo.

Wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao thamani ya elimu na uaminifu. Mtoto asitumiwe kuwaitea wazazi pesa, vile vile hiyo isiwe sababu ya kumzuia asifanye kazi.

MAFUNZO YA SURA HII KWANGU

Hapo kale, kulingana na desturi za Kiafrika, lilikuwa jambo la aibu kwa wazazi kukosa kuwalea watoto wao vizuri. Watoto walianza kujifunza walipokuwa babo wadogo kupitia kwa hadithi na vitendawili. Akina mama walishughulika na wasichana na akina baba walishughulika na wavulana. Lengo lao lilikuwa kuwatayarisha vijana hawa kwa maisha yao ya baadaye. Lakini siku hizi mtindo huu wa zamani umepuuzwa sana. Watoto wanaachwa kukua hivi hivi. Hii imewafanya wajifunze mambo ambayo hayafai kamwe.

Wazazi huwa wanawalaumu watoto mara kwa mara na kusahau kwamba wao wamesahau wajibu wao wa kuwafundisha tabia mbaya na njema. Je! wewe kama mzazi wa baadaye, unaweza kufanya nini ili kushinda shida hizi? Kumbuka kwamba Mungu ametuamuru tuwafundishe na tuwalee watoto wetu kwa adabu njema. Kwa hivyo ni lazima tuwe na maono na makusudi ya kutimiza amri ya Mungu. Wazazi hawapaswi kuogopa kuwafundisha watoto wao mambo fulani ya maisha. Kwa mfano, mama huona ugumu wa kumfundisha binti yake mambo yanayohusu unyumba, wala baba hamfundishi mwanawe. Woga kama huu umewafanya watoto wetu kutoelewa mambo wanayopaswa kujua hadi shida zinapotokea.

Shida nyingine ambayo wazazi wapya wanayo siku hizi ni kukosa maarifa ya mambo ya kuwafundisha watoto wao. Wana

SURA YA SITA

AMRI YA MUNGU KWA MKE

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza matarajio ya Mungu kwa mke.

SOMO KUTOKA: Waefeso 5:22-33; 1 Petro 3:1-2; Tito 2:3-5

VIFUNGU VYA LEO: Waefeso 5:22-33

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Kadhalika ninyi wake, watiini waume zenu; kusudi, ikiwa wako wasoliamini Neno, wavutwe kwa mwenendo wa wake zao, pasipo life Neno" (1 Petro 3:1).

KUSOMA SOMO

UTANGULIZI

Baada ya Bw. na Bi. Petro kuoana, baba ya Petro alimwambia kwamba aondoke nyumbani kwake na atafute mahali pa kuishi. Petro alimwambia baba yake amruhusu wakae hapo kwa mwezi mmoja tu, lakini baba yake alikataa. Kwa hivyo walienda katika mji mwingine ambako waliishi nyumbani kwa wazazi wa mkewe. Petro alianza kufanya kazi baada ya kuoana kwa muda wa mwezi mmoja. Alipaswa kwenda kazini na kumwacha mke nyumbani.

Mambo yalianza kubadilika katika mwezi wa pili wa ndoa yao. Kila wakati mume aliposema naye mke alimjibu kwa ukali. Chakula hakikuwa tayari alipotoka kazini. Mke hakuonyesha kumjali mumewe wala Mungu. Waligombana kila wakati badala ya kuwasiliana na kutatua shida zao. Walijitea shida nyingi. Kisha wakaanza kuishi hivyo.

Wasichana wanapaswa kujitayarisha kuwa wake na wavulana wanapaswa kujitayarisha kuwa waume. Mwelewe mtu huyo kabla ya kuoana, na ni muhimu kuweka malengo yenu.

MAELEZO

Amri ya Mungu kwa mke ni kumtii na kumheshimu mumewe. Neno kutii, linawezwa kusemwa lina maana ya kuwa mnyenyekevu, mpole na mtiifu.

Wake, katika kiabu cha Mwanzo wameciwa wasaidizi na wenzi wa waume zao. Katika Mwanzo 2:18 na Waefeso 5:22, Mungu anamwamuru mke kumtii mumewe jinsi anavyomtii Mungu. Pia, kifungu cha 33 kinasema kwamba ni lazima kila mke amtii mumewe. Wake wengi wameifanya heshima kuwa woga. Lakini tukielewa heshima kati ya wazazi, italeta usawa katika ndoa. Woga huleta utumwa.

Katika 1 Petro 3:1-2, kuna amri hiyo inayowataka wake wawatii waume zao. Inaongezea kwamba mwenendo wao mzuri utamsaidia mume ye yote ambaye hajiamwamini Yesu, kukata shauri. Kisha inasema kwamba hakuna haja mke kusema neno kwa mumewe ambaye si Mkristo. Mume huyo ataona maisha safi na ya kumcha Mungu ya mkewe Mkristo na kuvuliwa kumwamini Bwana.

Katika Tio 2:3-5, wazee wa kike wanaambiwa kuenenda vizuri na kuishi maisha matakaitu. Hawapaswi kuwa wasingizaji au wanaokunywa mvinjo - pombe. Ni lazima wafundishe yaliyo mema ili wawaongoze wanawake vijana kuwapenda waume na watoto wao.

Ni lazima wawe wenye kiasi, safi na wake wema ambao wanawatii waume zao. Wanapaswa kuishi maisha safi na makamilifu ili ujumbe wa Mungu usipate kudharauliwa. Vifungu hivi vyote vinazungumzia kuhusu mwanamke Mkristo,

kuwaokoa. Wanapaswa kujifunza habari za Yesu na kifo chake msalabani kwa ajili ya dhambi za wanadamu. Watoto wanapaswa kujifunza kumpenda Mungu na kutaka kumtumikia kwa sababu ya yale ambayo Yesu amewafanyia.

Tunasoma katika 1 Timotheo 3:4-5 kwamba ni lazima wazazi waisimamie nyumba yao vizuri na wawafanye watoto wao wawatii na kuwaheshimu.

Maandiko haya yote yanatusaidia kujua jinsi ya kuwalea watoto wetu ili wawe jinsi Mungu anavyotaka. Je! Wazazi watawataka nini watoto wao? Kusudi la kwanza kwa wazazi Wakristo kwa watoto wao linapaswa kuwa kuwaongoza kumjua Mungu na kumpokea Mwana wa Mungu, Yesu, awe Mwokozi wao. Watoto wanapaswa kujua kwamba Mungu ndiye aliyewaumba na akatoa mwanawe pekee awe Mwokozi wao. Kwa hivyo, watoto ni mali yake na wanapaswa kutafuta mapenzi ya Mungu kwa maisha yao. Tunapaswa kuwa na wajibu wa kuwafundisha watoto wetu Neno la Mungu kama watu wa Agano la Kale. Watakumbuka zaidi kile wanachojifunza wakiwa nyumbani. Wazazi wengi wanafikiri kwamba Shule na makanisa ndiyo yenye wajibu kufundisha na kuwalea watoto wao. Wanasahau kwamba watoto hukaa sana nyumbani kuliko kanisani. Pia, baadhi ya waalimu si Wakristo, hata ingawa huwa shuleni kwa saa nyingi, hawawafundishi watoto Neno la Mungu. Watoto hupata msingi imara wa maisha yao wakiwa nyumbani.

Watoto hujifunza kutokana matendo ya wazazi wao. Hujifunza haraka kwamba kitu fulani ni muhimu kwa wazazi na kitakuwa muhimu kwao. Watoto watajifunza kwenda kanisani, kutoa zaka na sadaka, kuomba kabla ya kula na kusoma Neno la Mungu ikiwa wazazi wao wanafanya hivyo. Viyoy hivyo, mtoto akona baba yake akikosa kuhudhuria ibada, ataamua kwamba kanisa si kitu muhimu kwake.

Siku moja wakati Paulo na rafiki zake walipokuwa wakirudi nyumbani kutoka shuleni, waliona matunda yaliyoiva shambani la Stefano. Walijaribiwa kwenda kuiba machungwa na maembe yaliyokuwepo shambani, lakini Paulo alikumbuka alivyoambiwa na wazazi wake. Aliwaambia rafiki zake wasiende kuiba lakini wao walisema kwamba hawatashikwa. Paulo alielekea nyumbani wakati rafiki zake wakienda kuiba matunda.

Vijana hawa walishikwa na mwenye shamba. Wakapigwa na kufukuzwa shuleni kwa wiki kadhaa. Paulo alishukuru mafundisho ya wazazi wake alipoendelea na masomo yake. Je! ni yupi kati ya vijana hawa ambaye ungependa awe mwanao?

MAELEZO

Waisraeli waliambiwa na Mungu kukumbuka amri zake. Waliambiwa wawafundishe watoto wao, wazirudie walipokuwa nyumbani, walipotembea njiani, wanapokaa na hata wakiwa kazini. Waliambiwa wazifunge mikononi mwao na mbele ya nyuso zao kama ukumbusho. Walipaswa kuziandika kwenye mimo (vizingiti) ya nyumba zao. Soma Kumbukumbu la Torati 6:4-9.

Hivi ndivyo amri hizi zingekuwa sehemu ya maisha ya watoto wao, kwamba watazifikiria kila wakati. Hawangesahau jinsi Mungu alivyowaamuru wakati walipotaka kujua. Watoto wangeweza kumtii Mungu vizuri kwa sababu walikuwa na mafundisho haya maishani mwao. Hawakuwa wameshirikiana na Mungu kama wazazi wao, kwa hivyo walihitaji msaada wa kuwawezesha kukumbuka amri zake.

Katika Waefeso 6:4, wazazi wameambiwa wasiwatendee watoto wao mambo ya kuwakasirisha. Bali wanapaswa kuwalea katika adabu na maonyo ya Kikristo. Watoto wanapaswa kujifunza mapema kwamba Mungu anawapenda na anataka

yule ambaye amempokea Yesu Kristo awe Bwana na Mwokozi.

Je! wasichana ambao baadaye watakuwa wake wanapaswa kufanya nini ili wawe jinsi Mungu anavyotaka? Tito 2:4 inasema, wafundisheni wasichana mema, "ili... wawapende waume zao, na kuwapenda watoto wao." Soma pia kifungu cha 5. Je! ni mambo gani mengine ambayo wasichana wanapaswa kufundishwa? Wanapaswa kuonyesha na mawazo mema. Wanapaswa kuiweka miili yao safi kwa ajili ya waume zao. Wanapaswa kujifunza jinsi ya kuitunza nyumba na jamaa yao, na ni lazima wawe wapole. Hivi ndivyo Neno la Mungu litakavyo heshimiwa.

MAFUNZO YA SURA HII KWANGU

Je! utafanya nini ili ujitayarishe kuwa mke au mume anayetarajiwa na Mungu? Jambo la kwanza ni kwamba, unapaswa kugeuka na kumfuata sasa, ikiwa humjamkubali Yesu awe Bwana na Mwokozi wako. Mambo mengine yote yatafuata baadaye. Ni vigumu mwanamke asiye Mkristo kujua na kuelewa amri za Mungu kwa wana wake. Hawaendi kanisani wala makundi wanawake na ushirika kwani wanafikiri kuwa ni kupoteza wakati. Wake kama hawa huwaitea jamaa zao shida kama mke wa Petro alivyofanya. Hawaoni wajibu wao katika jamaa. Watoto wao huwa wachafu na wana njaa mchana kutwa, nyumba ni chafu, na hakuna mtu wa kumpokea mume anapotoka kazini. Nyumba ya mke kama huyu hukumbwa na shida. Shida nyingi huletwa na mke kwa kukataa kutimiza wajibu wake.

Baadhi ya wanawake siyo mifano mizuri kwa wasichana. Wanawake kama hawa wamejiingiza katika vita vya maneno - wakidai haki zao bila kutaka kutimiza wajibu wao. Wanaweza kudai kwamba wao ni sawa na waume zao, lakini wanasahau heshima iliyoko kati ya mke na mume. Wake wanapaswa

kufanya kazi zao ili kuzisaidia jamaa zao kuishi vizuri. Hivyo basi, waume zao watafurahia kazi yao na hii itaimarisha uhusiano wao. Nao wanaweza kufanya kazi pamoja kama wasaidizi na si kama watumwa.

Jei unapanga kufanya nini nyumbani kwako kama mke atakayolewa? Jei kama mume, unatarajia nini kutoka kwa mke utakayemwoa? Kata shauri lako sasa ili uweze kuiti amri za Mungu juu ya jambo hili muhimu. Unapaswa kumwomba Mungu akusaidie kuwa mke mwema, yule atakayemtii, kumheshimu na kumsaidia mumewe. Au umwombe Mungu akusaidie umheshimu yeye kwa jinsi unavyomteenda mkeo. Mwenzi mwema ataonyesha kumjali mwenzake. Mke mwema anapaswa kuwa tayari kujadili na kutatua shida zinazowapata. Atamwomba mke awapo mbali na watoto wake. Utampendeza Mungu na kuwa tayari kumtumikia ukitayarisha nyumba yako jinsi hii. Jei unataka nyumba ya aina gani? Jei uko tayari kukubali wajibu wako kwa kuikuza nyumba kama hii?

KAZI YA KUFANYA

1. Sema Kifungu cha Kukumbuka, 1 Petro 3:1.
2. Mwombe Mungu kila siku akusaidie baada ya kuoa umti na kumheshimu mumeo, au akusaidie kuwa mume mpole na mwenye upendo.
3. Andika orodha ya mambo ambayo Mungu anatarajia kutoka kwa mume na mke.

wakati ujao mtakavyofanya kazi pamoja. Weka orodha hii mahali pazuri na mjadiliano na mchumba wako kabla ya kuoana.

3. Mwombe Mungu kuongoze kumpata mchumba ambaye mtashirikiana pamoja kwa utukufu wake.

SURA YA NANE

MALENGO YA WAZAZI KWA WATOTO WAO

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza mambo ambayo wazazi wanapaswa kuwatakia watoto wao.

SOMO KUTOKA: Kumbukumbu la Torati 6:4-9; Waeefeso 6:4; 1 Timotheo 3:4-5

VIFUNGU VYA LEO: Kumbukumbu la Torati 6:4-9; Waeefeso 6:4; 1 Timotheo 3:4-5

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee" (Mithali 22:6).

KUSOMA SOMO

UTANGULIZI

Paulo alikuwa mtoto wa pekee wa Andrea na Elizabeth. Kama wazazi walishughulikia maisha ya baadaye ya mtoto wao. Walitimiza wajibu wa kumfundisha na kumlea Paulo. Wazazi wote walimshauri mtoto huyo anayotarajiwa kufanya shuleni, nyumbani na katika jamii.

Paulo alipoanza shule akiwa na umri wa miaka saba alikuwa tayari ameamua kuwatii wazazi wake ikiwa wapo ama hawapo. Shule yake ilikuwa umbali wa maili mbili kutoka nyumbani, na barabara ya kwenda shuleni ilipitia kwenye shamba kubwa. Miti mizuri ilitoa matunda ya mazuri pale njiani.

Kiongozi wa nyumba hiyo ni Yesu Kristo, naye mume na mke wanayo haki sawa katika kukata mashauri.

Mume na mke wanapaswa kuomba na kusoma Neno la mungu pamoja kila siku. Pia, wanapaswa kufanya kazi pamoja. Pengine watakuwa na miradi ya kufanya pamoja. Wazazi wanapaswa kuwa na wakati wa kukaa na watoto wao na kufanya mambo wanayoyafurahia. Hii itakuza uhusiano wa jamaa na kuwasaidia kufanya kazi pamoja.

MAFUNZO YA SURA HII KWANGU

Katika ulimwengu huu wa sasa, watu wanajishughulisha sana kutafuta na kudumisha umoja. Umoja huu huanzia nyumbani wakati mume na mke wanapofunganishwa. Roho huyu wa umoja anawezwa kudumishwa katika kanisa, jamii na mwishowe ulimwenguni kwote.

Tukipata kanisa lenye nguvu na linalokua siku hizi, tutagundua kwamba washiriki wake wana umoja nyumbani kwao. Mungu anataka watu wake wawe na umoja, na wafanye kazi pamoja kama kitu kimoja. Waume na wake wanapaswa kuelewana bila uchoyo, kuwasiliana vizuri, kwa matumizi mazuri ya pesa na kwa kumwomba Mungu kila siku kuiongoza nyumba yao. Malezi na kuwafundisha watoto ni wajibu wa wazazi wote wawili.

Mwombe Mungu akuongoze kukuza nyumba ambayo itamheshimu. Wakati huu unapofanya mipango yako ya baadaye, kata mashauri ya mambo utakayofanya wakati huo, na kisha utekeleze matakwa yako. Mungu na akusaidie unapopanga nyumba yako ya baadaye.

KAZI YA KUFANYA

1. Andika orodha ya mambo utakayofanya ili kuwa na nyumba yenye furaha. Andika pia jinsi wewe na mchumba wako wa

SURA YA SABA

USHIRIKIANO WA MUME NA MKE

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitajifunza kwamba ni lazima mume na mke wafanye kazi pamoja nyumbani.

SOMO KUTOKA: Wafilipi 2:1-4; Waefeso 4:2-3

VIFUNGU VYA LEO: Wafilipi 2:1-4; Waefeso 4:2-3

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Hali mnanenyekeana katika kicho cha Kristo" (Waefeso 5:21).

KUSOMA SOMO

UTANGULIZI

Waume na wake huomba na kutarajia maisha ya furaha yenye amani, upendo na umoja katika ndoa yao. Lakini wakati mwingine haifanyiki hivyo. Jel hutokea kipingamizi gani?

"Nitaolewa na Yusufu hata wazazi wangu waseme nini!" Esther alisema, "Yeye ni tajiri." Alifikiri kwamba watakuwa na ndoa nzuri ya amani. Yusufu alipoenda kuwajulisha wazazi wa msichana, walikataa kwa kuwa walifahamu ubaya wake pale kijijini. Alikuwa amekwisha waacha wake wawili!

Wazazi wa Esther walimwita chumbani na wakamwambia sababu wanazofikiria kuwa si vyema kuolewa na Yusufu. Jamaa yote hawakutaka aolewe naye, lakini Esther alisisitiza kwamba amemchagua Yusufu.

Yusufu alibadili tabia yake baada ya arusi. Akasema, "Esther, kumbuka kwamba uko hapa kuonekana, wala si kusikizwa." Alimkanya asitumie kitu cho chote pale nyumbani bila ruhusa. Sheria hizo zilikuwa nyingi sana na kali; hadi Esther akashindwa kuzitii zote. Mwishowe, alipaswa kurudi kwa wazazi wake aliowapuza baada ya miezi mitano.

Jei unapaswa kufikiria mambo gani unapochagua mchumba ili mwe na ndoa ya furaha? Jei unawezaje kuipanga nyumba yenye furaha?

MAELEZO

Wafilipi 2:1-4 inatupa baadhi ya mashauri jinsi ya kujibu maswali haya. Kifungu cha kwanza kinaonyesha kwamba faraja yetu itakuwa katika Kristo. Yeye ndiye atatafariji wakati wa shida, na atatusaidia katika yote tutakayofanya kwa ajili yake. Roho wake atakuwa pamoja nasi kila wakati kutusaidia katika shida za kila siku.

Halupaswi kufanya kitu cho chote kwa sababu ya uchoyo au kwa kutaka sifa, lakini tunapaswa kuwa wanyenyekevu tukiwafikiria wenzetu kuwa bora zaidi yetu. Tunapaswa pia kujua anayopenda mwenzetu na kutiana moyo. Ni muhimu kwa walioana kuwa na nia moja, upendo mmoja, malengo sawa na kusudi moja katika ndoa hiyo. Mume na muke watataka kumpendeza Yesu katika ndoa yao ikiwa wanamtegemea kwa uamuzi wa maisha yao. Watatafuta msada wake katika kukata mashauri na watafurahia umoja katika ndoa yao. Ikiwa mmoja wapo katika jamaa ni Mkristo, atataka mapenzi ya Mungu ayafanywe nyumbani kwao. Iwapo mmoja wao si Mkristo atataka nyumba yao iongozwe kwa njia ya kidunia. Watu hawa wawili hawana lengo moja, na tayari kuna shida katika ndoa hiyo. Kila mmoja anashughulika kusudi tofauti, na haiwezekani kuwa na amani.

Biblia ina suluhisho kamili kwa shida hii. Tafadhali tufungue katika 2 Wakorintho 6:14. Kifungu hiki kinasema, "Msitungwe nira pamoja na wasioamini...." Hii ina maana kwamba vijana wanapaswa kupanga vizuri kabla ya kuoa. Wanapaswa kumchagua mtu anayemwamini Mungu kama wao. Mkristo hapaswi kuoa yule asiye mwamini Mungu, kwa kuwa watatunganihwa pamoja. Nyumba kama hii haiwezi kuwa na

amani, kwa sababu hawashughuliki lengo moja. Wanaweza kuomba pamoja kama wanafanya kazi pamoja, naye Mungu atawaongoza katika njia nzuri aliyowachagulia.

Vifungu hivyo vya Wafilipi vinatwambia pia kwamba tusifanye kitu cho chote kwa majivuno. Kila mmoja anapaswa kumfikiria mwingine kuliko anavyojifikiria mwenyewe. Uamuzi haupaswi kufanywa kulingana na matakwwa ya mtu, lakini kila mmoja anapaswa kufikiria mahitaji ya mwenzake.

Wafeso 4:2-3 inatwambia kwamba tunapaswa kuwa wanyenyekevu, wapole na wavumilivu. Tunapaswa kuonyesha upendo kwa kuvumiliana ka kuelewana. Jei waume na wake wanahitaji nini tena ili kushirikiana pamoja katika jamaa zao mbali na yale tuliyosoma katika Maandiko ya Biblia?

Wanapaswa kuwasiliana kwa njia nzuri na kamifitu. Wakati fulani watu husema jambo fulani wakiwa na maana nyingine. Jambo hili ni la hatari sana katika ndoa. Kila mmoja anapaswa kuwa na nafasi ya kujadili mambo yanayowahusu. Ni lazima aseme wazi, na wote wanapaswa kuamua pamoja kwa faida yao.

Mume na mke wanapaswa kupanga pamoja matumizi ya pesa zao. Pesa ndicho chanzo cha kukosana au kubishana kati ya jamaa. Jamaa nyingi wanateseka kwa sababu ya matumizi mabaya ya pesa. Watoto wanahitaji chakula, nguo na karo ya shule. Tendo hili halipaswi kuwepo. Pesa haiitakuwa chanzo cha shida ikiwa watapanga pamoja jinsi ya kutumia pesa zao na kisha wafuate mpango huo.

Uhusiano wa waume na wake unawezwa kulinganishwa na mafuga ya kupikia. Jiwe moja ni mfano wa Yesu, la pili mume na la tatu mke. Mawe yote matatu yanahitajika ili kuleta furaha katika jamaa. Chuungu kitaanguka kama moja halipo.